# MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

# Muongozo wa Utambuzi wa Vifaa vya Mawasiliano ya Simu

UMETOLEWA NA TCRA – JULAI 2024

# MUONGOZO YA UTAMBUZI WA VIFAA VYA MAWASILIANO YA SIMU, 2024

Hati Namba: TCRA/DIA/TIM/GUD-MDD/004

| Imeidhinishwa na: | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| **Dkt. Jabiri K. Bakari** | **Mkurugenzi Mkuu** | [signature] | 10/07/2024 |

# Yaliyomo

Orodha ya Vifupisho .......................................................................................4

1. Jina ........................................................................................ 5
2. Maombi ........................................................................................ 5
3. Tafsiri ........................................................................................ 5
5. Taratibu za Uendeshaji wa CEIR ........................................................ 7
6. Kushughulikia IMEI Zilizorudufiwa........................................................ 8
7. Malalamiko ya Wateja ........................................................................ 8
8. Kuzuia Udanganyifu na Faragha........................................................... 8
9. Marekebisho........................................................................................8

## Orodha ya Vifupisho

| | |
|---|---|
| CDRs | Kumbukumbu za taarifa ya matumizi ya mawasiliano |
| CEIR | Rejista Kuu ya Utambuzi wa Vifaa ya mawasiliano ya simu |
| ESN | Namba za utambuzi za vifaa katika mtandao wa simu |
| GSM | Mfumo wa Kimataifa wa Mawasiliano ya Simu za Mkononi |
| GSMA | Shirika la Mfumo wa Kimataifa wa Mawasiliano ya Simu |
| ICT | Teknolojia za Habari na Mawasiliano |
| IMEI | Utambulisho wa Kimataifa wa Vifaa vya Mawasiliano |
| IMSI | Utambulisho wa mteja mtandaoni, inatumika wakati wa kubadilishana taarifa za mteja kimtandao |
| ITU | Shirika la Mawasiliano la Kimataifa |
| EIR | Rejista ya Utambuzi wa Vifaa vya Mawasiliano ya Simu |
| KYC | Kumfahamu Mteja Wako |
| MSISDN | Utambulisho wa mteja mtandaoni |
| NIN | Namba ya Utambulisho ya Taifa |
| RB | Taarifa ya Polisi |
| SIM | Moduli ya utambulisho wa mteja |
| TAC | Namba ya Utambulisho ya Kifaa cha mawasiliano ya simu |

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

### 1. Nukuu

Muongozo huu utanukuliwa kama Muongozo wa utambuzi wa Vifaa vya mawasiliano ya simu, 2024.

### 2. Matumizi

Muongozo huu unatumika kwa wamiliki wa leseni za huduma za mtandao wanaotoa huduma za mawasiliano ya simu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 3. Tafsiri

Katika Muongozo huu, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo: -

**"Chama cha Mfumo wa Kimataifa wa Mawasiliano ya Simu"** kifupi GSMA, maana yake ni chama cha kimataifa cha waendeshaji wa mawasiliano ya simu za mkononi za GSM;

**"Huduma ya Mtandao"** maana yake ni huduma ya kusafirisha taarifa kwa njia ya sauti au sauti nyingine, intaneti, ujumbe mfupi wa maandishi au picha kwa kutumia nishati ya elektromagnetiki inayoongozwa au isiyoongozwa;

**"Kifaa cha simu"** maana yake ni kifaa kinachoshikika kwa mkono ambacho kinatambulishwa kipekee na namba tambulishi wa kimataifa au namba za usajili wa kielektroniki na kinachotumiwa na wateja kwa ajili ya mawasiliano;

**"Kitabu cha taarifa"** kwa kifupi RB, maana yake ni taarifa inayotumika katika taratibu za Jeshi la Polisi la Tanzania, ikijumuisha namba ya kumbukumbu kwa simu iliyopotea, kupatikana au kuharibika;

"**Kuorodheshwa kwenye orodha nyeupe**" maana yake ni mchakato wa kuanzisha upya simu mpya au kuiwasha tena simu ya mkononi iliyopotea au kuibiwa ili kupata huduma za mtandao kutoka kwa watoa huduma wa huduma za mtandao baada ya simu hiyo kupatikana;

**"Leseni ya Huduma ya Mtandao"** maana yake ni leseni ya mawasiliano ya kielektroniki inayompa mtoa huduma haki ya kutoa huduma moja au zaidi za mtandao;

**"Mamlaka"** maana yake ni Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania namba 12 ya mwaka 2003;

**"Mfumo wa Kimataifa wa Mawasiliano ya Simu"** maana yake ni teknolojia ya kidijitali ya simu kwa ajili ya utoaji wa huduma za mawasiliano ya sauti, jumbe fupi za maandishi na intaneti;

**"Moduli ya Utambulisho wa Mteja (SIM)"** maana yake ni mzunguko jumuishi unaokusudiwa kuhifadhi kwa usalama utambulisho wa kimataifa wa mteja wa simu za mkononi (IMSI) na ufunguo unaohusiana unaotumika kutambua na kuthibitisha wateja kwenye vifaa vya simu za mkononi;

**"Mteja"** maana yake ni mtu anayepokea huduma ya mtandao chini ya makubaliano na au kulingana na masharti ya mtoa huduma wa huduma ya mtandao;

**"Mtoa huduma wa Huduma ya Mtandao"** maana yake ni mtoa huduma wa huduma ya mtandao;

**"Namba ya Kimataifa ya Orodha ya Wateja wa kifaa cha Simu"** au kwa kifupi MSISDN maana yake ni namba inayotolewa kwa mteja;

**"Namba za usajili wa Kielektroniki"** kwa kifupi ESN, maana yake ni namba ya kipekee inayotumiwa na mtandao wa mawasiliano ya kielektroniki kutambua kifaa kimoja cha mawasiliano ya kielektroniki;

**"Namba tambulishi iliyoigwa"** maana yake ni namba tambulishi ya vifaa vya mawasiliano ya simu ambavyo vimebadilishwa au kunakiliwa;

**"Namba tambulishi za vifaa zilizorudufiwa"** maana yake ni namba tambulishi ya kifaa cha mawasiliano ya simu ambayo inatumiwa na zaidi ya kifaa kimoja cha simu kwa wakati mmoja kwenye mtandao wowote, bila kujali kama namba tambulishi husika ni halisi (asili) au si halisi;

**"Namba tambulishi zisizokubalika"** maana yake ni namba tambulishi za vifaa vya mawasiliano ya simu zinazokiuka au zilizoko nje ya namba zilizokubaliwa za GSMA TACs;

**"Namba za ugawaji wa aina ya kifaa (TAC)"** maana yake ni sehemu ya awali ya tarakimu nane ya namba tambulishi ya vifaa vya mawasiliano yenye tarakimu 15 inayotumika kutambua vifaa vya simu kwa kipekee;

**"Orodha ya Kijivu"** maana yake ni orodha ya vifaa vya mawasiliano ya simu ambavyo vimezuiliwa au kuruhusiwa kwa muda kupata huduma za mawasiliano;

**"Orodha nyeupe"** maana yake ni orodha ya namba tambulishi ikiwemo namba za wateja na namba tambulishi ya vifaa kimataifa zilivyorekodiwa na mmiliki wa huduma ya mawasiliano ya kielektroniki ambapo hazipo kwenye orodha nyeusi au kijivu;

**"Orodha ya nyeusi"** maana yake ni orodha yenye namba tambulishi ya vifaa vya mawasiliano ya simu zilizoripotiwa kama zimepotea, kuibiwa au kuharibiwa;

**"Rejista kuu ya utambulisho wa vifaa vya mawasiliano ya simu"** kwa kifupi CEIR, maana yake ni kanzidata ya kielektroniki inayoshikilia namba tambulishi ya vifaa vya mawasiliano ya simu, zikiwa katika orodha tatu ambazo ni orodha nyeupe, orodha nyeusi na orodha kijivu;

**"Rejista ya Utambulisho wa Vifaa mawasiliano ya simu"** kwa kifupi EIR, maana yake ni kanzidata ya kielektroniki ambayo inashikilia namba za utambulisho wa mawasiliano ya simu (IMEI au ESN) ipo katika orodha za rangi tatu kama inavyopatikana ndani ya miundombinu ya mwenye leseni ya huduma za mtandao;

**"Uchambuzi wa namba tambulishi iliyoigwa"** maana yake ni mchakato unaofanywa ili kubaini namba tambulishi ya vifaa vya mawasiliano ya simu ambavyo vimebadilishwa au kunakiliwa;

**"Utambulisho wa Kimataifa wa Mteja wa Simu"** kwa kifupi IMSI, maana yake ni utambulisho wa kipekee unaotumiwa na waendeshaji wa mitandao ya simu za mkononi kutambua mteja katika mitandao yao;

**"Utambulisho wa Kimataifa wa Vifaa vya Simu"** kwa kifupi IMEI, maana yake ni namba tambulishi zinazotumika kutambua simu za mkononi katika mitandao ya Mfumo wa Kimataifa wa Mawasiliano ya Simu za Mkononi (GSM); na

**"Vifaa bandia vya mawasiliano"** maana yake vifaa bandia vya mawasiliano ambavyo namba zake za utambulisho hazipo kwenye kandidata ya utambulisho wa vifaa vya mawasiliano ya GSMA.

**4. Malengo ya Muongozo**

Kama sehemu ya kushughulikia changamoto zinazohusiana na usambazaji usio sawa wa idadi ya vifaa vya simu kati ya maeneo ya mijini na vijijini, kuna haja ya kufuatilia na kuweka kumbukumbu za idadi ya vifaa, ukuaji na usambazaji wa vifaa ili kuelewa uwezo wa watumiaji katika kutumia huduma za teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT) ikijumuisha huduma za serikali.

Aidha, wizi wa vifaa vya simu na ulaghai vimekuwa changamoto na kilio cha umma kwa watumiaji wengi nchini. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kupitia Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Rejista Kuu ya Utambulisho wa Vifaa) za mwaka 2018 inasimamia rejista Kuu ya Utambulisho wa Vifaa ambayo inarahisisha ukusanyaji wa 'triplets' za vifaa vya simu pamoja na kuweka kwenye orodha nyeusi, nyeupe au kijivu vifaa vya simu vilivyoripotiwa kuibiwa, kupotea, kuharibika, kutokubalika au ulaghai sokoni.

Miongozo hii inakusudia kutoa taratibu za kugundua vifaa vya simu katika mitandao ya mawasiliano, hivyo kuwezesha usimamizi wa vifaa vya simu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Malengo mahususi ya Muongozo huu ni pamoja na: -: -**

i. Kutoa utaratibu wa ufuatiliaji idadi na matumizi ya vifaa vya simu nchini;
ii. Kurahisisha udhibiti wa matumizi ya vifaa vya simu vilivyoripotiwa kuibiwa, kupotea, kuharibiwa, visivyokidhi viwango au vilivyojihusisha katika shughuli za udanganyifu;
iii. Kusaidia kubaini changamoto za matumizi ya huduma za mawasiliano na hatua zinazohusiana ili kutatua changamoto hizi;
iv. Kusaidia kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwa watumiaji katika sekta ya mawasiliano;
v. Kutoa utaratibu wa kuripoti vifaa vilivyopotea, vilivyoibiwa, kuharibiwa, visivyokidhi viwango au vilivyojihusisha katika shughuli za udanganyifu kwa mtoa huduma wa huduma za mtandao kwa ajili ya kuweka kwenye orodha nyeusi; na
vi. Kusaidia kudhibiti uingiaji wa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki nchini, mchakato wa kuvithibitisha na kuwalinda watumiaji.

## SEHEMU YA PILI

## UENDESHAJI WA REJISTA KUU YA UTAMBULISHO WA VIFAA

**5. Taratibu za uendeshaji wa rejista kuu ya utambulisho wa vifaa**

Taratibu za uendeshaji wa rejista kuu ya utambulisho wa vifaa utakuwa kama ifuatavyo: -

a) Mtoa huduma anapaswa:

i. kuhakikisha anaweka taratibu za ndani ili kuruhusu wafanyakazi walioidhinishwa pekee ndiyo wanaofanya kazi kwenye rejista ya utambulisho wa vifaa (EIR);
ii. kuhakikisha mifumo ya rejista ya utambulisho wa vifaa (EIR) inaunganishwa na mfumo wa rejista kuu ya utambulisho wa vifaa (CEIR) wakati wote kwa kutuma taarifa za kidijiti kwa muda uliowekwa na Mamlaka;
iii. kuweka utaratibu wa kuthibitisha utambulisho wa mtu anayeripoti namba tambulishi ya

kifaa iliyoripotiwa;

iv. kuoredhesha kwenye orodha nyeusi au ya kijivu namba tambulishi ya vifaa vilivyoripotiwa na kuwasilisha orodha hiyo kwa muundo ulioainishwa na Mamlaka;

v. kuoredhesha kwenye orodha nyeupe namba tambulishi, inatakiwa kufanywa na mtoa huduma aliyeanzisha mchakato wa kuiorodhesha namba tambulishi kwenye orodha nyeusi au ya kijivu na inapaswa kukamilishwa ndani ya saa moja (1) kutoka wakati wa kuripoti;

vi. kuhakikisha mtu anayeripoti namba tambulishi ili kuorodhesha kwenye orodha ya nyeusi, kijivu au nyeupe anapewa namba ya kumbukumbu kwa ajili ya ufuatiliaji;

vii. anaweka utaratibu wa kuangalia namba tambulishi iliyoripotiwa kwa kuorodhesha kwenye orodha nyeusi, kijivu au nyeupe;

viii. kuchakata taarifa za vifaa na kuijulisha Mamlaka idadi ya vifaa vilivyochakatwa;

ix. kuwasilisha "triplets" kila siku hususani orodha nyeupe, ya kijivu na nyeusi kwa muundo ulioainishwa na Mamlaka; na

x. kuhakikisha namba tambulishi za vifaa zisizokidhi viwango haziruhusiwi kuunganishwa na mitandao.

b) Mamlaka kila siku itachakata taariza za vifaa iliyopokelewa kutoka kwa watoa huduma na kutengeneza taarifa nyingine maalum na kutuma kwa watoa huduma wote saa saba mchana na saa saba usiku.

## SEHEMU YA TATU
## NAMBA TAMBULISHI ZA VIFAA ZILIZORUDUFIWA

### 6. Kushughulikia namba tambulishi za vifaa zilizorudufiwa

Katika kushughulikia namba tambulishi za vifaa zilizorudufiwa, Mtoa huduma atapaswa: -

a) kuongeza namba ya utambulisho wa kitaifa (NIN) kwenye "triplets" ili kuandaa taarifa yenye utambulisho wa kimataifa wa vifaa vya simu (IMEI), utambulisho wa kimataifa wa mteja wa simu (IMSI), namba ya kimataifa ya orodha ya wateja wa kifaa cha simu (MSISDN) na utambulisho kitaifa (NIN);

b) kufanya uchambuzi wa namba tambulishi iliyoigwa kutoka utambulisho wa kimataifa wa mteja wa simu (IMSI) zilizounganishwa mara mbili au zaidi na utambulisho tofauti wa kitaifa (NIN) na kuzitambua kama namba zilizorudufiwa;

c) kufanya uchambuzi ili kubaini eneo la utambulisho wa kimataifa wa mteja wa simu (IMSI) wa namba husika;

d) kuorodhesha namba zilizorudufiwa katika orodha ya nyeusi zilizobainika katika maeneo tofauti;

e) kutuma ujumbe mfupi wa maandishi kwa wateja walio kwenye orodha nyeusi ikibainisha sababu ya kuorodhesha vifaa vyao kwenye orodha hiyo; na

f) kuwasilisha orodha ya namba tambulishi zilizorudufiwa katika muundo ulioainishwa kwa Mamlaka.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA JUMLA

**7. Malalamiko ya Wateja**

Malalamiko yanayotokana na uendeshaji wa mfumo wa rejista ya utambulisho wa vifaa vya mawasiliano ya simu (EIR) yatashughulikiwa kulingana na masharti ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ulinzi wa Watumiaji) za mwaka 2018.

**8. Kuzuia Udanganyifu na Faragha**

a) Mtoa huduma atashirikiana kwa nia njema kuzuia matukio ya shughuli zisizo za kimaadili, ushindani na udanganyifu;

b) Kama matukio ya udanganyifu yatagundulika, watoa huduma wanaohusika watashirikiana ili kubaini na kutatua udanganyifu huo; na

c) Utambuzi wa vifaa vya mawasiliano ya simu utafanywa kwa kuzingatia sheria za ulinzi wa taarifa binafsi na faragha.

**9. Marekebisho**

Muongozo huu unaweza kufanyiwa mapitio ya mara kwa mara na Mamlaka kadri itakavyoona inafaa kwa maendeleo ya sekta ya mawasiliano.



## Wasiliana Nasi

**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania**
**Jengo la Mawasiliano, 20 Barabara ya Sam Nujoma,**
**S.L. P 474, Postikodi 14414 Dar es Salaam**
**+255 22 2199760 - 9 / +255 22 2412011 - 2 / +255 784558270 - 1**